# Saa 15 za chekechea (kindy) ya bure

**Chekechea ni kwa saa 15 kwa wiki, wiki 40 kwa mwaka na bila malipo.**

**Shule ya chekechea inatolewa kwa njia tofauti katika huduma tofauti. Kwa huduma kadhaa, saa 15 za chekechea za bure zinaweza kutolewa katika siku mbili au tatu, na matunzo ya ziada hulipiwa kwa ziada. Ikiwa mtoto anahudhuria chekechea katika mpangilio wa matunzo ya siku ndefu, matunzo ya ziada yanaweza kulipwa kwa sehemu na Ruzuku ya Huduma ya Watoto ya Serikali ya Australia (Australian Government Child Care Subsidy).**

